# VIPENGELE VYA UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI ANDISHI

## Yaliyomo

- Fasili ya fasihi
- fasili ya uhakiki
- Vipengele vya uhakiki wa kazi za fasihi
    - **Fani**
    - **Maudhui**

Fasihi ni sanaa inayo tumia lugha katika kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyo kusudiwa (Taasisi ya Elimu Tanzania, 1996). Haji (1983:30) fasihi ni sanaa itumiayo maneno ili kutoa picha halisi ya mwanadamu akiwa maishani mwake; mahusiano yake na viumbe wengine, migogoro yake na mazingira, shida zake, raha zake, matumaini yake na jinsi anavyopiga hatua katika maendeleo yake. Fasihi ni kazi ya sanaa itoayo maudhui yake kwa kutumia lugha ya kutamka au kuandika ili kufikisha ujumbe kwa jamii. Fasihi ni sanaa inayotumia lugha ili kufikisha ujumbe kwa jamii fulani (tunuzakiswahili.blogspot.com). Fasihi ni kazi ya sanaa inayotumia maneno katika kufikisha ujumbe kwa jamii, kuburudisha, kuonya, kukejeri, na hata kukashifu (www.shuledirect.com). Fasihi ni sanaa inayotumia ishara (maneno au matendo) kutoka picha halisi ya maisha kwa njia bunifu na inayofuata mpangilio maalumu na lugha ya kifasaha ili kuiathiri hadhira husika (Ntarangwi, 2004). Hivyo basi fasihi ni kazi ya sanaa itoayo maudhui yake kwa kutumia lugha ya kutamka au kuandika ili kufikisha ujumbe kwa jamii.

Uhakiki ni kitendo cha kutathimini, kueleza, kuainisha na kutoa maoni juu ya kazi fulani ya fasihi kwa kuongozwa na kaida maalumu (Ntarangwi, 2004). Uhakiki ni uchunguzi wa kazi ya kifasihi kwa makini na kwa utaalamu. Uchunguzi wa aina hii huchunguza uchanganuzi, fasiri, uelezaji, ufafanuzi, tathimini na utoaji wa kauli ya kijumla (Wamitila, 2002). Uhakiki ni utathmini, ufasili na uainishi wa kazi za fasihi, haumaanishi kutafuta makosa ya kazi hiyo(Peck & Coyle). Kwa hiyo, Uhakiki ni kitendo cha kuchambua, kutathmini na kuainisha kazi ya fasihi ili kuona ubora na udhaifu wa kazi hiyo kwa kutumia kaida au vigezo husika vya fani na maudhui.

Katika uchambuzi na uhakiki wa kazi za fasihi kuna vipengele vikuu viwili ambavyo ni;

## MAUDHUI

**Maudhui** ni kile kinachosemwa katika kazi ya fasihi (Ntarangwi, 2004). **Maudhui** ni jumla ya mawazo yote yanayozungumzwa pamoja na mtazamo wa mwandishi juu ya mawazo hayo. Maudhui hujumuisha mawazo pamoja na mafunzo mbalimbali yaliyomsukuma msanii hadi akatunga na kusainii kazi fulani ya kifasihi (www.shuledirect.com). **Maudhui** ni jumla ya mawazo yote yanayozungumzwa katika kazi ya fasihi. Hivyo tutaanza kwa kuchambua vipengele vya maudhui ambavyo hujumuisha dhamira, ujumbe, migogoro, mtazamo, na falsafa.

**Dhamira** ni ile jumla ya maana anayoivumbua mwandishi aandikapo, na jumla ya maana anayoitambua msomaji katika usomaji wake (Wamitila, 2002). Dhamira hutumiwa kurejelea mada ya kazi fulani au ujumbe au lengo la kazi hiyo. Kifasihi kuna aina mbili za dhamira yaani dhamira kuu na dhamira ndogondogo\

- Dhamira kuu ni kiini cha kazi ya fasihi, ni wazo kuu, ni jambo linalomsukuma msanii kuandika kazi yake ili aweze kuufikisha ujumbe wake kwa hadhira.
- Dhamira ndogondogo, ni mawazo madogomadogo ambayo hujenga dhamira kuu.

Mifano ya dhamira ni kama zifuatazo kutoka katika kazi mbalimbali za kifasihi ambazo ni;- Kutoka katika Tamthiriya ya *Amezidi* kilicho andikwa na *Said Mohamed* dhamira zilizomo ni kama vile Ulevi, mwandishi ameizungumzia katika ***uk 50*** anasema "*wanakunywa wisky…"* . Na dhamira nyingine ni kama vile Umasikini na Matabaka ***uk 60***. Tamthiriya ya *Nguzo Mama* iliyoandikwa na *Penina Mhando* ameelezea dhamira mbalimbali kama vile dhamira ya Ukombozi wa mwanamke, kama ilivyoelezwa na mwandishi kwa kumtumia "Bi Nane; *Basi tusikilizane. Mnajua Nguzo Mama haiwezi kusimama mpaka tuivute kwa kamba"*. Pia katika riwaya ya *Kufirika* mwandishi *Shaban Robert* ameonesha dhamira kuu ni Ukombozi wa kiutamaduni. Kiujumla riwaya ya *kufikirika* inajadili harakati zinazofanywa na Utu Busara za kupambana na tamaduni zilizopitwa na wakati. Pia mwandishi amejadili dhamira ndogondogo kupitia wahusika lukuki ambao amewatumia katika riwaya hii, Dhamira hizo ni kama zifuatazo: Suala la uongozi, Suala la ugumba na utasa,

Mgogoro: ni hali ya kutokuelewana baina ya pande mbili yaani mtu na mtu, mtu na kikundi au mtu mwenyewe na nafsi yake. Migogoro ni mivutano na misuguano mbalimbali katika kazi za fasihi. Migogoro inaweza kuwa kati ya wahusika, familia zao au matabaka yao. Migogoro hii inaweza kugawanywa katika vipengele vifuatavyo;

- mgogoro wa nafsi,
- mgogoro wa kijamii,
- mgogoro wa kiuchumi
- Mgogoro wa kisiasa.

Mfano mwandishi *Shaaban Robert* katika riwaya yake ya *Kufikirika* ameonesha migogoro mbalimbali kama vile mgogoro wa kiuchumi, kijamii, kisiasa, utamaduni na mgogoro wa nafsi. Tukianza na ***mgogoro wa kiuchumi***, mwandishi ameonyesha jinsi nchi ya kufikirika ilvyoyumba kiuchumi kutokana na mali zote za nchi zilivyotumika katika kumtibu mfalme na malkia na mwishowe shughuli za nchi zilisimama (*uk.8-12).* Pia kuna ***mgogoro wa kijamii***, mwandishi ameonyesha mgogoro wa mfalme na malkia kwa kukosa mtoto, kwakua walijiona hawana umuhimu katika jamii ingawa walikua na mali nyingi. (*uk.1-6).* Katika kitabu cha Tamthiliya ya *Amezidi* kilicho andikwa na *Said Mohamed* kuna mgogoro kati ya *Mari* na *Zidi*, ambapo Mari aliahidiwa mali nyingi na Zidi lakini hakutimiziwa. Mfano, *Mari* anasema, "….*ziko wapi, kanzu mpya za kujimwaga? Ukasema mabegi sita yananingojea mimi… na manukato… na mambo kemkem ya kujipodoa…." (uk. 23).* Pia mgogoro kati ya *Ame* na *Zidi* unaojitokeza pale wanapogombania nyama, kwa mfano mwandishi anasema,"*Nyama inawaanguka na wao wanavaana na kupigana*…." (uk.70). Pia katika Riwaya ya *Kusadikika* iliyo andikwa na Shaaban Robert, ameonesha migogoro mbalimbali kama vile, migogoro ya kijamii. Mfano wa migogoro ya kijamii ni mgogoro wa *Sapa* na *Salihi* uliotokea baada ya Sapa kuomba upofu kutokana na tamaa ya Salihi kutamani vitu vya Sapa (*uk 30).* ***Mgogoro wa Kisiasa.*** Huu ni mgogoro unaowahusisha wanaharakati wazalendo walioongozwa na karama dhidi ya serikali na viongozi wa nchi ya Kusadikika. Wanaharakati hao walihitaji mabadiliko na walichoshwa na uonevu wa viongozi wao, mgogoro huu ndio uliopelekea wananchi kuishia kifungoni pindi walipojitolea kudai mabadiliko. Migogoro mingine ni ule wa nafsia na Kiuchumi**.**

**Ujumbe** ni funzo na maadili yaliyokusudiwa na mtunzi yaifikie jamii aliyoilenga kufikisha kazi yake ya fasihi. Katika riwaya ya *Kufikirika* iliyoandikwa na Shaaban Robert kupitia dhamira mbalimbali zimeweza kutuibulia ujumbe ufuatao; *Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu*. Mfano wananchi wa kufikirika walikuwa na umoja katika kufanikisha ustawi wa nchi yao hali kadhalika watu wa kufikirika walikuwa na umoja na ushirikiano katika kufanikisha mfalme wao anapata mtoto. *Kwenye upendo, umoja na ushirikiano hakuna vurugu na matatizo mbalimbali*. Ustawi wa nchi ya Kufikirika umetokana na umoja na ushirikiano waliokuwa nao, na *Jamii isijiegemeze katika imani za kimila na kitamaduni tu bali iangalie upande mwingine.* Hii inatokana na ukweli kwamba wanakufikirika walikuwa hawaamini masuala ya hospitali badala yake walikuwa wanaamini mambo ya kimila na kitamaduni. Pia katika Riwaya ya *Kusadikika* iliyoandikwa na *Shaaban Robert* ameonesha ujumbe kama, *Uongozi mbaya unachangia kwa kiasi kikubwa kukwamisha maendeleo ya wananchi*, *kuwa na tamaa na viongozi kujali maslahi binafsi kunapelekea hali duni ya wananchi walio wengi* na *Viongozi wanapaswa kuthamini haki za wananchi wanaowatumikia*. Pia kutoka katika Tamthiriya ya *Nguzo Mama* iliyoandikwa na *Penina Mhando* ameonesha ujumbe mbalimbali kama vile, *Umoja ni nguvu, Umuhimu wa ukombozi wa mwanamke*, na *Uongozi bora ni chachu ya maendeleo.*

**Falsafa,** kiujumla falsafa ni mchujo wa welekeo wa mawazo muhimu yajitokezayo kila mara katika kazi mbalimbali za msanii ( Senkoro, 2011). Falsafa ni imani na mwelekeo wa mwandishi kuhusu maisha. Kutoka Riwaya ya *Kusadikika* iliyoandikwa na *Shaaban Robert* falsafa ya mwandishi ni ya *"wema hushinda ubaya"*, amedhihirisha hili kupitia mhusika Karama aliyechorwa kama mtu mwema dhidi ya Majivuno aliyechorwa kama mtu mbaya. Kwa taswira hii Karama amewakilisha wema wote katika jamii ya wasadikika na Majivuno anawakilisha wabaya wote katika jamii hiyohiyo. Pia katika kitabu cha Riwaya za *Rosa Mistika, Mzingile na Nagona* ziliyoandikwa na Kezilahabi falsafa yake ni *"Maisha hayana maana".* Pia kutoka katika Tamthiriya iliyoandikwa na *Penina Mhando* ya *Nguzo Mama* mwandishi anaamini kwamba *"Mwanamke ukimwezesha anaweza".*

Msimamo wa mwandishi, msimamo ndio uwezo wa kuwatofautisha wasanii wawili wanaotunga kazi za fasihi zilizo na kiini na chimbuko moja ( senkoro, 2011). Katika riwaya ya *Kufikirika* mwandishi *Shaaban Robert* anaonekana kuwa na msimamo wa kiyakinifu. Kwa mujibu wa mwandishi anaona katika kipindi cha sayansi na teknolojia mila na tamaduni za zamani zisipewe

nafasi. Kutoka katika riwaya ya *Kusadikika* msimamo wa mwandishi *Shaaban Robert* ni wa kimapinduzi, kwani anaonesha jinsi jamii ilivyopaswa kujituma tena kwa ujasiri, kupigania haki na mabadiliko ya wananchi wote. Katika tamthiriya ya *Nguzo Mama* msimamo wa mwandishi, *Penina Mhando* ni wa kimapinduzi, kwani anajaribu kuiaminisha jamii na kuibadirisha kifikra kutoka kutomwamini na kutomthamini mwanamke na kuanza kujenga imani juu yao. Mfano amemchora mhusika *Bi- Nane* kama mtu mwenye msimamo na mpenda maendeleo.

# FANI

**Fani** katika fasihi ni ule ufundi wa kisanaa anaotumia msanii katika kazi yake (Senkoro 2011). Fani ni ufundi wa msanii katika kuumba umbo la kazi ya fasihi kutokana na ubunifu wake. Fani ni ufundi ambao msanii anautumia katika kufikisha ujumbe kwa jamii. Katika fani msomaji anatakiwa kuzingatia;

- Muundo au mtiririko(ploti) wa kazi
- Mtindo alioutumia mwandishi katika kazi yake
- Lugha - mwandishi ametumia lugha namna gani
- Madhari
- Wahusika - jinsi mwandishi alivyo wasawili wahusika wake
- Usimulizi wa kazi za fasihi

**Wahusika** ni binadamu wanaopatikana katika kazi ya kifasihi na ambao wanasifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi na kifalsafa ambazo hutambulishwa na wanayoyasema (mazungumzo) na wanayoyatenda (matendo) (Wamitila, 2002). **Mhusika** katika fasihi ni kiumbe cha hadithini kilichobuniwa na msanii ili kuendeleza hoja na maudhui yake katika kazi yake (Ntarangwi, 2004). **Wahusika** ni viumbe hai au visivyo hai ambavyo vinawakilisha watendaji halisi katika maisha ya kila siku ya jamii husika katika kuonyesha wasifu wa ndani na nje kama vile hali ya kusononeka mhusika, furaha au tabia fulani katika jamii inayotuzunguka. Hivyo wahusika huelezea hali halisi ya maisha ya jamii. Iwe mitaani, iwe sehemu za kazi, iwe shuleni na kwingineko ambako kunahusisha mikusanyiko ya watu wa tabia tofauti tofauti. Mhusika husaidia katika kuendeleza mada nzima anayoizingatia msanii hususa kwa kufululiza vitushi na visa mbali mbali katika kazi ya msanii ili kuwafikia wasomaji au wasikilizaji wake. Mhusika hupewa maneno, dhana, na hulka ambazo ni muhimu katika kujenga hadithi, dhamira, na maudhui ya kazi

ile. Wahusika wanakusudiwa kutenda matendo, tabia au matukio halisi katika mazingira halisi. **Wahusika** wamegawanyika katika makundi makuu mawili ambayo ni wahusika wakuu na wahusika wasaidizi.

- **Wahusika wakuu** ni wale wanaobeba dhamira kuu katika kazi ya fasihi. Hawa ndiyo vipaza sauti vya mwandishi. Wahusika hawa huonekana kuanzia mwanzo wa hadithi hadi mwisho wake.
- **Wahusika wadogo** au **wasaidizi** ni wale ambao wanajitokeza hapa na pale katika kazi ya fasihi ili kukamilisha ulimwengu wa kazi hiyo. Wahusika hawa hutumiwa na mwandishi katika kukuza dhamira. Wahusika wadogo wamegawanyika katika aina mbalimbali. Wako *wahusika bapa, Mviringo,Kinyago, Jumui, Batili, Foili na wahusika Kikalagosi.*

Mfano katika Riwaya ya *Kufikirika* mwandishi *Shaaban Robert* amewatumia wahusika mbalimbali katika kuibua au kuunda dhamira zake. Baadhi ya wahusika aliowatumia ni kama *Mfalme*, huyu alikuwa ndiye kiongozi au mfalme wa nchi ya Kufikirika ambaye aliongoza vema na alikuwa mtu mwenye huruma na upendo na watu wake. Hali kadhalika mfalme alikuwa ni jasiri na mzalendo aliyepigania haki. *Malkia*, huyu alikuwa ni mke wa mfalme ambaye pia alikuwa anasumbuliwa na tatizo la utasa, ni mwanamke mvumilivu na mwenye subira, hivyo mwandishi kwa kumtumia mhusika Malkia ameibua dhana ya utasa na uvumilivu. *Utu busara ujinga hasara*, ni mhusika aliyeibua dhamira nyingi katika riwaya hii ya kufikirika, alikuwa ni mtu makini na mwenye upeo mkubwa katika kufikiria mambo. Huyu ndiye aliyetabiri kuzaliwa kwa mtoto wa mfalme, baadaye akawa mwalimu wa mtoto wa mfalme na baadaye akajiingiza katika ukulima *(uk 49).* Pia katika Tamthiliya ya *Nguzo Mama* mwandishi *Penina Mhando* amewachora wahusika mbalimbali ili kufikisha ujumbe aliokusudia kwa msomaji. Wahusika hao ni kama vile, *Bi-Pili* ambaye alikuwa ni mpishi wa pombe, ni mpenda maendeleo na pia ni mke wa *Sudi* na mlezi wa familia. *Bi-Nne* huyu ni mhusika mkuu, ni mwenye wivu asiyependa maendeleo ya wenziwe, na ni mwenyekiti wa kamati ya mashauri. *Bi- Nane* ni msomi, ni mpenda maendeleo, na ni mvumilivu. Kitabu kingine ni Riwaya ya *Amezidi* mwandishi *Shaaban Robert* amewatumia wahusika kama, *Ame* na *Zidi* hawa ni wahusika wakuu katika kazi hii. Wahusika wengine wadogowadogo ni *Mari, Joice, na Jane*. Kutoka katika tamthiliya ya *Kwenye Ukingo Wa Thim* kilicho andikwa na *Ibrahim Hussein* yeye amewatumia wahusika wafuatao ili kufikisha ujumbe

kwa wasomaji wake, *Abert* na *Marther* ambao ni wahusika wakuu katika tamthiliya hii na wengine wadogowadogo ni kama vile;- *Kriss, George, Ridia, Jine,* na *Stella.*

**Muundo** hutokana na umbo na mpango wa kazi ya fasihi; kwa hiyo hapa ndipo tutapata katika ushairi wa Kiswahili, mashairi yenye miundo mbalimbali iainishwayo na idadi ya mistari (vipande/mishororo) katika kila ubeti, mathalani mashairi ya uwili, utatu, unne (Senkoro, 2011) Muundo katika kazi ya fasihi muundo ni mpango na mtiririko wa kazi hiyo kwa upande wa visa na matukio (Senkoro 2011). **Muundo** ni namna matukio katika kazi ya fasihi yalivyopangwa na kuleta mtiririko wa kazi husika ya fasihi. Muundo ni mtiririko wa kazi ya fasihi kwa upande wa visa na matukio. Kinachozingatiwa hapa ni jinsi mwandishi alivyopanga kazi yake mfano sura na sura, kisa na kisa au tukio na tukio. Muundo unaweza ukawa wa aina zifuatazo.

- Muudo sahili.- Muundo wa moja kwa moja
- Muundo wa urejeshi-Muundo wa kuanzia mwisho-kati-mwanzo au kinyume chake.
- Muundo wa duara
- Muundo changamani- huwa na matukio/hadithi tofauti tofauti ndani ya hadithi au kisa kimoja.
- Muundo mpalaganyiko.

Hivyo katika riwaya ya *Nagona* mwandishi *E. Kazilahabi* ametumia muundo wa "Rejea" ambapo mwandishi ameanza na kisa cha mbele katika kazi yake. Kutoka katika Tamthiliya ya *Nguzo Mama* mwandishi ametumia muundo wa "moja kwa moja" (sago) ambapo amepanga matukio au visa vyake kwa mtiririko kutoka onesho la kwnza hadi la nne. Kitabu kingine ni kile cha *Kufikirika* mwandishi *Shaaba Robert* ametumia muundo wa "moja kwa moja" ambapo amesimulia kitabu mwanzo hadi mwisho. Kwa kuigawa kazi yake katika sehemu ndogondogo, kwakuzipa vichwa vya habari kama vile *Mfalme, Waganga*, *Matokeo ya utabiri*, *Mtoto wa mfalme na Kafara*. Pia sura ya tano ameigawa katika sehemu kuu mbili na kuipa jina la *Baraza na Gereza*.

**Mtindo**, katika kazi ya fasihi ni ile nama mbayo msanii hutunga kazi hiyo na huipa sura ambayo kifani na kimaudhui huainisha kanuni au kawaida zilizofuatwa kama ni zilizopo (za kimapokeo) au ni za kipekee (senkoro 2011). **Mtindo** ni upekee wa uundaji wa kazi ya fasihi na hutofautiana baina ya msanii mmoja na mwingine kulingana na hisia za msanii huyo. Utofauti huo unaweza

kujitokeza kwenye matumizi ya nafsi, uteuzi wa msamiati, mwanzo na mwendelezo wa kazi yake, usimulizi wa mwandishi, uchanganyaji wa tanzu mbalimbali za fasihi, kama vile kuingiza kipengele cha wimbo katika kazi ya fasihi andishi. Katika Tamthiliya ya *Nguzo Mama* mwandishi *Penina Mhando* ametumia mtindo wa "majibizano (dialojia) (*uk 36- 37)*, mtindo wa "monolojia" (*uk 13 na35)*, mtindo wa nafsi zote tatu mfano; *Nikianza kuyasimulia* nafsi ya kwanza, *Nawewe wajua kupika* nafsi ya pili, na ile ya tatu ambayo ni *Wakaanza kuinua*. Katika Riwaya ya *Kufikirika* Mwandishi *Shaaban Robert* katika kazi yake hii ametumia mtindo wa "masimulizi" yaani amesimulia matukio yote katika mtiririko unaofaa, pia "nafsi zote tatu zimetumika", hali kadhalika mwandishi ametumia "ushairi" (*uk 18-19)*. Pia ametumia mtindo wa kutoa maana ya meneno magumu mwishoni. Pia katika Riwaya ya *Kusadikika* Mwandishi *Shaaban Robert* ametumia mitindo mbalimbali katika kazi hii kama vile, ametumia "maswali" hasa katika sehemu ya mwisho ya kitabu, ametumia "diolojia" kati ya Sapa na Salihi (*uk. 29)*, ametumia "masimulizi" kwa kiasi kikubwa, na matumizi ya "nafsi ya pili na tatu umoja na nafsi ya tatu wingi" sehemu kubwa ya kazi yake.

**Mandhari** huwa ni sura ya mahali hususa jinsi panavyoonekana katika hali halisi ya maisha. Mtunzi anaweza kutumia mandhari kueleza mazingara halisi ya kisa anachosimulia katika kazi yake. Mathalani, mtunzi anaweza kutuchorea mandhari ya pwani kwa kushughulikia vitu kama vile upwa na ziwa, minazi, nyumba za makuti n.k. Jambo hili huleta hali ya ufasaha katika utunzi (Ntarangwi, 2004). **Mandhari** ni ile arki au elementi ambayo hutufichulia wapi na lini ambapo matukio fulani yalifanyika (Wamitila, 2002). **Mandhari** ni mahali ama wakati tukio la kifasihi lilivyobuniwa na kutendeka na msanii na hivyo hufanikiwa kujenga hisia ya msomaji au msikilizaji ama mtazamani kulingana na kazi yake ya fasihi aliyoiandaa. Mandhari ni sehemu ambayo kazi ya fasihi ilitendeka, inatendeka au itatendeka. Kazi ya fasihi iwayo yote ile lazima iendane na mandhari husika. Aidha mada au jambo linalozungumzwa sharti iendane na sehemu au mahali ambapo tukio hutokea. Madhari hutumika kulejelea wakati na sehemu matukio ya msuko hutokea.

Kwa mfano katika riwaya ya *kufikirika* mwandishi *Shabani Robert* ametumia mandhari ya kufikirika, kwani hata nchi inayozungumziwa ni ya Kufikirika, pia nchi zilizopakana na nchi ya Kufikirika nazo ni za kufikirika. Pia mwandishi ametumia muktadha halisi kama vile Gerezani, Nyumbani kwa Mfalme, Bustanini *(uk 1)* na Shambani. Kupitia mandhari hizi mwandishi, *Shabani Robert* ameibua dhamira mbalimbali. Katika kitabu cha *Kusadikika* mwandishi ametumia

mandhari ya *Kufikirika* ambayo haiwezi kuonekana kwa macho ya kawaida kwani ni nchi inayoelea angani. Pia ametumia mji wa Sadiki na mipaka au pande sita zinazopakana na nchi hii za Kaskazini, Mashariki, Kusini, Magharibi, Ardhini na Mbinguni. Pia kitabu cha tamthiliya ya *Nguzo Mama* mwandishi ametumia *mazingira halisi* kwani ni ya kijijini.

**Matumizi ya lugha** ni namna ambavyo msanii ameteua na kupangilia tamathali za semi kama sitiari, tashbiha, takriri, tashihisi na tafsida, methali, misemo, taswira,nahau, lugha za kigeni na kadhalika.

**Matumizi ya lugha**, hujumuisha jinsi mtunzi alivyotumia lugha katika kuwasilisha kazi yake. Matumizi ya lugha hujumuisha misemo, nahau, methali na tamathali za semi. Mifano ya matumizi ya lugha kutoka kazi mbalimbali za kifasihi ni kama ifuatayo;- Katika kitabu cha riwaya cha *Kufikirika* mwandishi ametumia lugha ya, **Methali**, methali zilizotumika katika riwaya hii ni kama vile, *nyumba ya mgumba haina matanga (uk 5), mwenye haya hazai (uk 6), asiye kubari kushindwa si mshindani" (uk 27).* Kutoka katika kitabu cha *Kusadikika* mwandishi *Shaaban Robert* ametumia methari kama, *Kitanda usichokilalia hujui Kunguni wake, Msiba wa kujitakia hauna kilio, Lila na fila hawatangamani.* Pia katika tamthiliya ya *Nguzo Mama* mwandishi ametumia methari zifuatazo katika kazi yake, *Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu (uk 30), Lamgambo likilia lina jambo (uk 4), Aso mwana aeleke jiwe (uk 4).* **Misemo**, Katika riwaya ya *Kufikirika* misemo iliyotumika ni kama ifuatayo;- *Dunia haifichi siri (uk 23), maisha ni kama kuwa katika bahari ( uk 24).* Kitabu cha *Nagona* mwandishi ametumia misemo kama *Fikra hufumba mboni za urazini (uk 14)* Pia kutoka katika tamthiliya ya *Nguzo Mama* mwandishi ametumia misemo kama, *Ukilikoroga pumba nakula utalila (uk 26), Utakufa kibudu (uk 23), Akachanganya ulimi (uk 57).* Katika kitabu cha *Kusadikika* mwandishi ametumia misemo mbalimbali kama vile, *kumtosa mshitakiwa katika bahari ya maangamizi.* **Tamathali za semi**, haya ni maneno ambayo hutumiwa na wasanii wa fasihi ili kutia nguvu katika maana, mtindo na hata sauti katika maandishi au kusema. Pia tamathali za semi hutumika ili kupamba lugha au mazungumzo. Mfano katika riwaya ya *Kusadikika* mwandishi Shaaban Robert ametumia tamathali mbalimbali kama zifuatavyo:- **Tashibiha,** katika riwaya hii tashibiha zilizojitokeza ni kama vile *kichwa chake kilishindiliwa kama gunia (uk 29), Sauti ya waafrika ni kali kama ile ya radi (uk 6), Waliweza kunusa kama mbwa mwitu (uk 8), Akili yake kali kama wembe (uk 38), Maswali aliyamimina kama maji (uk 29).* Kutoka katika kitabu cha Amezidi mwandishi ametumia tashibiha

kama vile; *Mkono wangu mrefu kama ule wa Shetani (uk 8).* Kitabu cha *Mzingile* kuna tashibiha kama *Uogaji wangu haukuwa kama wa ndege (uk 7).* Kitabu cha *Nguzo Mama* mwandishi ametumia tashibiha kama *Amevaa kama mkulima wa bara (uk 24), Wanasagwa kama mbuzi (uk 32), Anatembea kama amepigwa na bumbuazi (uk 8).* **Sitiari** ni tamathali ya semi ambayo hulinganisha vitu viwili au zaidi bila kutumia maneno kama, au mithili ya. Katika tamthiliya ya *Amezidi* mwandishi Said Mohamed ametumia sitiari kama vile; *Tuwe simba basi (uk 72).* Katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, mwandishi *Kezilahabi* ametumia sitiari kama vile "*Huyu ni baba yako*." (uk.12) pia "*Ujamaa ni mzuri*.' (uk.112) **Takriri** ni tamathali ya semi ambayo neon hujirudiarudia kwa lengo la kusisitiza jambo fulani. Katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* mwandishi *Kezilahabi* ametumia sitiari katika sehemu mbalimbali mfano *"Haa! Haa! Haa!"(uk.12),* "*Mauti mauti*" *(uk.17).* Pia katika tamthiliya ya *Amezidi* mwandishi *Said Mohamed* ametumia takriri mfano "*mumu mumu" (uk.75), "Joto…joto...ndani joto na nje joto" (uk.36).*

**Tashihisi,** hapa vitu visivyo na sifa walizonazo watu hupewa sifa hizo. Katika kitabu cha *Nagona* mwandishi amezionesha kama ifuatavyo; *Bonde la hisia (uk 16), bonde la mvi (uk 18).* Kitabu cha *Vuta N`Kuvute* mwandishi ametumia tashihisi zifuatzo; *Nuru ya jua iliingia kwa hamaki chumbani mle na ilikashifu uchafu wote wa chumba kile (uk 49).* Kitabu cha *Kufikirika* mwandishi *Shaaban Robert* ametumia tashihisi zifuatazo, *Sauti ya ndege waliokuwa wakiimba matawini kwa kuagana na mchana ilikuwa na simanzi masikioni (uk 1).* Katika kitabu cha *Kusadikika* tashibiha zilizotumika ni kama vile; *Giza limezalo nuru na ufupisho uoni wa macho***,** *Wakati una mabawa kama ndege (uk. 11).* Katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, *Kezilahabi* pia ametumia tashihisi mfano "*kila jiwe walilokalia liliwaambia samahani umekalia bega langu."(uk.32)*

**Mubalagha**, ni tamathali ya semi ambayo hutia chumvi au hukuza jambo. Katika riwaya ya *Kufikirika* mwandishi ametumia mbinu hii katika ***(****uk 11****)*** *siku hiyo kuni, mkaa, na mafuta yote yalikwisha kwa kuchoma hirizi hizo, moshi mwingi uliruka juu ukatanda katika hewa kama wingu kubwa la mvua.*

**Matumizi ya lugha za kigeni,** hizi ni lugha azitumiazo mwandishi katika kazi yake ya kifasihi ili kufikisha ujumbe na kumburudisha msomaji wa kazi yake. Mfano wa lugha hizo zilivyo tumika katika kazi za kifasihi ni kutoka kitabu cha *Amezidi* mwandishi ametumia maneno ya lugha ya kiingereza kama *"How do you do? All right! (uk 60)", Cheers! (uk 58), Entertainment (uk 49).* Pia

katika kitabu cha *Mzingile* mwandishi ametumia maneno ya lugha ya kiingereza kama *well done! (uk 40).* Kitabu cha *Nguzo Mama* mwandishi ametumia maneno ya lugha ya kiingereza kama vile, *My God, Degree.* Aidha katika riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo mwandishi Kezilahabi ametumia lugha ya Kiingereza, mfano "*Welcome back" (uk.88). "Security (uk.89 - 90)." Snow cap" (uk.62)*

**Pia lugha ya picha**, waandishi wengi wa kazi za kifasihi hutumia lugha za picha ili kupunguza au kuficha baadhi ya mambo yasionekane dhahiri kwa mlengwa mwenyewe, au kuwakilisha tabia za watu katika jamii. Mfano kutoka katika kazi za kifasihi ni kama vile;- Katika kitabu cha *Nagona* mwandishi ametumia lugha ya picha kama *Kamasi, na funza (uk 16), vinyesi (uk 19), nyuki (uk 56).* Kitabu cha *Mzingile* mwandishi ametumia lugha ya picha kama *Mjusi (uk 46).* Kutoka kitabu cha *Nguzo Mama* mwandishi ametumia *kamba, nguzo mama.*

Kwa ujumla uchambuzi na uhakiki wa kazi mbalimbali za kifasihi humsaidia msomaji wa kazi husika ya kifasihi kuielewa au kupata mwanga fulani juu ya kazi husika aisomayo. Aidha kazi ya uhakiki hufanywa na mhakiki wa kazi ya fasihi ambaye ndiye hufanya kazi kubwa ya kuchanganua kazi mbalimbali za kifasihi ili ziweze kumrahisisihia msomaji kuzielewa kwa ufasaha kazi husika.

---

**MAREJEO**


Ameir, I.H (1983) *Misingi ya Nadharia ya Uhakiki*. Dar es Salaam: Tuki

Hussein, E.(1988). *Kwenye Ukingo wa Thim,* Nairobi,Oxford University Press East Africa Ltd.

Kezilahabi, E. (1990) *Nagona*, Dar es Salaam, Dar es Salaam University Press.

Kezilahabi, E. (1991) *Mzingile*, Dar es Salaam,Dar es Salaam University Press.

Kezilahabi, E. (2007) *Dunia Uwanja wa Fujo,* Nairobi, Vide Muwa Publishers

Mhando P. (1982) *Nguzo Mama*, Dar es Salaam, Dar es Salaam University Press.

Mohamed S.A (1995) *Amezidi*, Dar es Salaam, East African Educational Publishers.

na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI).

Ntarangwi, M. ( 2004). *Uhakiki Wa Kazi Za Fasihi*. Augustana College, Rock Island, IL612

Publishers Ltd.

Robert, S (1991) *Kufikirika*, Dar es salaam, Mkuki na Nyota Publishers.

Robert, S. (1991*) Kusadikika*, Dar es Salaam, Mkuki na Nyota Publishers.

Senkoro, F.E.M.K (2011) *Fasihi*, Dar es salaam, KAUTTU.

TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. (Toleo la Pili). East Africa: Oxford University Press

Wamitila K. W, (2002), *Uhakiki Wa Fasihi Misingi Na Vipengele Vyake*, Nairobi, Phoenix